ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera
22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni
23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake

28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe.Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
33. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
34. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
35. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
38. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani
39. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake
40. Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Jimbo la Wawi
41. Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Jimbo la Shaurimoyo
43. Mhe. Hassan Khamis Hafidh	-	Jimbo la Welezo
44. Mhe. Hidaya Ali Makame	-	Nafasi za Wanawake
45. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)	-	Jimbo la Mtoni
46. Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Jimbo la Paje
47. Mhe. Khadija Omar Kibano	-	Jimbo la Mtambwe
48. Mhe. Machano Othman Said	-	Jimbo la Mfenesini
49. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti	-	Jimbo la Mtopepo
50. Mhe. Makame Said Juma	-	Jimbo la Kojani
51. Mhe. Maryam Thani Juma	-	Jimbo la Gando
52. Mhe. Masoud Abrahman Masoud	-	Jimbo la Bububu
53. Mhe. Miraji Khamis Mussa	-	Jimbo la Chumbuni
54. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha	-	Jimbo la Mtambile
55. Mhe. Mohamed Said Mohamed	-	Jimbo la Mpendae

56. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
57. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
58. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
59. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
60. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
61. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
62. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
63. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
64. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
65. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
66. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
67. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni
69. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake
70. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi
71. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu
72. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Salma Mussa Bilal - Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Shaib Said Ali - Jimbo la Chonga
75. Mhe. Simai Mohammed Said - Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Sira Ubwa Mamboya - Uteuzi wa Rais
77. Mhe. Suleiman Makame Ali - Jimbo la Ziwani
78. Mhe. Suleiman Sarahan Said - Jimbo la Chakechake
79. Mhe. Tatu Mohamed Ussi - Nafasi za Wanawake
80. Mhe. Ussi Yahya Haji - Jimbo la Mkwajuni
81. Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Jimbo la Fuoni
84. Mhe. Zaina Abdalla Salum - Nafasi za Wanawake
85. Mhe. Zulfa Mmaka Omar - Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem - Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Tatu - Tarehe 25 Novemba, 2016

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Naibu Spika (Mgeni Hassan Juma) alisoma dua

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe naomba kidogo tutafanya marekebisho yale maswali ambayo Mhe. Waziri wa Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, tutaanza nayo mwanzo kutokana na dharura isiyoweza kuepukika, halafu baada ya hapo tutaendelea na maswali mengine.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 88

Udhamini wa Masomo kwa Askari wa Idara Maalum

Mhe. Zaina Abdalla Salum: Aliuliza:
Kama tunavyojua kwamba mfanyakazi yeyote anapochukua masomo ya Elimu ya Juu yaani *degree* kuongeza ujuzi wa kazi yake, hulipiwa masomo hayo na serikali kwa kupitia Wizara au Idara yake anayoifanyia kazi.
Kuna Askari wa Idara Maalum za SMZ ambao wamechukua masomo ya elimu ya juu yaani (*Degree*). Kwa mfano Chuo cha Mafunzo wanajilipia wenyewe kupitia mishahara yao ambayo haikidhi mahitaji ya familia zao na gharama za masomo yao.

(a) Je, huoni kwamba unawavunja moyo na imani kuwa askari hawa kwa kuitumikia nchi yao kwa uaminifu na mapenzi makubwa.
(b) Je, Serikali kupitia Wizara yako inawafikiria vipi askari hawa kuwapatia fedha hizo ili wakalipe madeni yao ya Chuoni.
(c) Serikali kupitia Wizara yako ni lini hasa fedha hizi zitakabidhiwa kwa askari hawa wanaosoma ili kuondosha usumbufu baina yao na Wakuu wao wa kazi.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Alijibu:
Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 88 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, suala la mafunzo kwa wafanyakazi wa serikali ni moja kati ya masuala yanayopewa kipaumbele ili kuongeza ufanisi na ujuzi katika kazi. Kwa kuzingatia hilo, Chuo cha Mafunzo kinafanya kila kilicho ndani ya uwezo wake kuona wafanyakazi wake wanapata fursa hii. Hata hivyo, kwa kuwa mwamko na mahitaji ya kwenda kusoma ni mengi ikilinganishwa na uwezo wa Chuo. Katika hali hii, Chuo cha Mafunzo kimekuwa kikichukua hatua ya kusaidia sehemu ya gharama za masomo ili askari wengi wapate fursa hii. Hatua hii wanajuulishwa askari kabla hawajajiunga na masomo yao ili kuepuka malalamiko baadae. Kwa yale mafunzo yanayohitajika na Chuo cha Mafunzo, askari wanaohudhuria mafunzo hayo hulipiwa gharama zote. Kwa kutambua uwezo uliopo na kwa utaratibu huu ninaamini bado askari wataendelea kutumia fursa iliyopo ya kujiongezea maarifa bila ya tatizo.

(b) Kama nilivyoeleza katika kifungu cha (a) Chuo cha Mafunzo kitaendelea kuwalipia askari wake wote walioko masomoni kwa kadiri hali ya fedha itakavyoruhusu, na kwa wale ambao walikwenda masomoni kwa kufuata utaratibu niliokwishaueleza awali.

(c) Kuhusu ni lini, Mhe. Naibu Spika, naomba nimjibu Mwakilishi kwamba dhamira na nia ya serikali kwa wale wanafanya kazi wanaosoma kwa kufuata utaratibu wa Chuo basi fedha hizo zitapatikana pale hali ya kifedha itakaporuhusu.

Mhe. Zaina Abdalla Salum: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa nyengine tena ya kuuliza swali la nyongeza katika Wizara hii.

Katika hii Idara Maalum ya Vikosi vya SMZ kuna vitengo vya sheria, vikiwa vinajulikana ni Idara ndogo za sheria, lakini vitengo hivi viko chini ya uteuzi wake yeye mwenyewe Mhe. Waziri husika, vitengo hivyo vinajishughulisha na kazi za kutetea haki na kushughulikia kesi mbali mbali za kiaskari pamoja na wananchi wengine kwa mfano Chuo cha Mafunzo, kitengo hicho kipo na kimeteuliwa na kiongozi wake mkuu ni Mwenyengome Begani. Lakini kwa masikitiko makubwa kitengo hicho kinapotaka kufanya shughuli zake za kufuatilia kesi hakina hata usafiri ule wa baskeli wa kufuatilia kesi hizo.

a) Je, Mhe. Waziri haoni kwamba anadhoofisha utendaji wa kazi hizo.
b) Ana mpango gani katika kutafutia usafiri kitengo hicho.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, naomba nimuombe Mwakilishi swali alilioliuliza ni swali ambalo kidogo linahitaji umakini mkubwa naomba swali hilo tumjibu kwa maandishi.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, lakini kama inawezekana ningekuomba dakika moja au nusu dakika kidogo nina neno langu nataka kusema ikiwa haiwezekani basi niendelee na swali.

Mhe. Naibu Spika: Unasemaje Mheshimiwa?

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Ninakuomba kama nusu dakika tu kidogo nina suala ambalo halihusiani na swali la maulizo.

Mhe. Naibu Spika: Kama halihusiani na swali ambalo lipo lililoulizwa huwezi kuuliza. Unajua Kanuni ...

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nakushukuru, nilikuomba tu Mheshimiwa kama haiwezekani naendelea na swali.

Mhe. Naibu Spika: Uliza swali ambalo linahusiana na kinachoulizwa swali la msingi.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mimi nilikuwa namuuliza Mheshimiwa kwamba kila Idara inakuwa inawapeleka wanafunzi wake au inawapeleka wafanyakazi wake katika kujisomea masuala tofauti tofauti. Nilikuwa namuuliza Mhe. Waziri ni fani gani ambazo anawapeleka wafanyakazi wake kwenda kuzisomea kwa staili ya kazi yake na kuendana na hali halisi ya wakati.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, ukweli ni kwamba katika Chuo cha Mafunzo kuna fani ambazo zinahitajika katika taasisi ile ambazo ni mojawapo zinaweza kusaidia katika kutekeleza ufanisi wa majukumu ya kila siku. Hata hivyo, katika majibu ni kwamba fani ambazo mara nyingi zinakuwa zinatolewa pale au wanaruhusiwa wanafunzi au wafanyakazi waende kujisomea ni mfano fani ya *health sciences, public administration, labor technicians, human resource, secretarial, law, procurement,* na kadhalika, ahsante.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo tu la nyongeza. Kwanza nimpongeze Mhe.

Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo na sisi yametutia moyo kwa juhudi za serikali hasa kwa kwenda kuwasomesha wafanyakazi wetu.

Katika majibu alikiri kwamba Chuo cha Mafunzo kinawapeleka wafanyakazi kusoma kwa maana wanafuatana na ile *training program*. Swali langu ni kwamba, katika mwaka wa bajeti 2015/16 Chuo cha Mafunzo katika *training program* yake kilipanga kusomesha wafanyakazi wangapi, na wangapi walifanikiwa katika kuwaingiza Chuoni na kuwasomesha katika ule mpango ambao unatokana na *training program* yake.

Mhe. Naibu Waziri Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, ni kweli katika mpango wa Wizara kupitia taasisi hii ilipanga katika kipindi cha 2015/16 kuwapa mafunzo wafanyakazi wake. Nataka nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba jumla ya wafanyakazi 19 walipatiwa mafunzo katika kipindi hicho ambao kwa mchanganuo wanawake walikuwa 7 na wanaume walikuwa 12 jumla walikuwa ni wafayakazi 19 ambao ndio waliopatiwa mafunzo katika kipindi hicho, ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kuongezea majibu ambayo yamejibiwa na Mhe. Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

Kwanza nataka nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake ambayo ameyajibu katika maswali yote, swali la msingi na maswali matatu ya nyongeza moja lilikuwa na (a) na (b) lililoulizwa na Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis, na jengine lililoulizwa na Mhe. Suleiman Sarahan Said na jengine lililoulizwa na Mhe. Miraj Khamis Mussa.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nataka niwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe kwa kuuliza maswali yenye viwango.

Ni kweli kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri kwamba taasisi yoyote ya serikali inakuwa na *training program* kwa ajili ya kuendeleza wafanyakazi wake. Hapa niwafahamishe Waheshimiwa Wawakilishi pale inapotokea kwamba kuna mfanyakazi amechukua kozi ya masomo bila ya kuzingatia *training program* ambayo imewekwa na taasisi, ndipo pale taasisi inapoelemewa na mzigo wa kuweza kuwasaidia na kuwasomesha.

Hata hivyo Chuo cha Mafunzo kimekuwa kikijitahidi katika kuhakikisha kwamba wale wote ambao wapo kwenye *training program* yake kwa zile kada ambazo tumeamua tuzifundishe kwa wakati ule, Chuo cha Mafunzo kimekuwa kikichukua juhudi hiyo na kuhakikisha kwamba wanafunzi hao wanasoma na hawapati matatizo ya kufukuzwa ndani ya vyuo vyao.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ambayo ameyasema Mhe. Naibu Waziri kuhusu suala la (a) na (b) la Mhe. Mwantatu ambalo aliahidi kulileta kwa maandishi. Kwa faida ya Baraza lako Tukufu naomba nitoe ufafanuzi na majibu kama hivi ifuatavyo:-

a) Mhe. Naibu Spika, kutokuwa na chombo cha usafiri katika kuwapeleka wafanyakazi wa kitengo cha sheria kufuatilia matukio ya askari sio kudhoofisha bali ni uwezo halisi. Hata hivyo Chuo cha Mafunzo kinazo gari za *pool* pale mwanasheria au mtu mwengine yeyote anapotaka kufuatilia kazi na haja hiyo ikiwepo, basi Chuo cha Mafunzo hufanya hivyo kama zinavyofanya taasisi nyengine za serikali.

b) Kuna mpango gani wa kuweza kuliondosha tatizo hilo? Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba Ofisi yangu kupitia Idara zote maalum za serikali inao mpango madhubuti katika mwaka ujao wa fedha, kuhakikisha kwamba tatizo la usafiri katika Idara zetu maalum za SMZ linamalizika, na hivyo wafanyakazi wa Idara maalum za SMZ kufanya kazi zao kwa ufanisi kama ilivyokusudiwa. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Nam. 156

Mpango wa Kuendeleza Eneo la Darajani

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Aliuliza:-

Serikali imekuwa katika mpango kabambe wa kuendeleza eneo la Darajani *(Darajani Coridor)* na hatua zimeshaanza kuchukuliwa. Kumekuwa na taarifa kuwa katika uendelezaji huo Skuli mbili kongwe za Darajani na Vikokotoni zitabomolewa kwa ajili ya kupisha ujenzi wa maduka makubwa ya biashara *(malls).* Kwa kuwa nchi nyingi hujenga maduka makubwa ya Biashara nje ya mji hasa katika miji mipya ili kutanua fursa za biashara na maendeleo ya miji mfano Dar es Salaam maduka hayo yamejengwa *Mlimani City*, aidha Mji wa Dubai wamejenga nje ya Mji.

(a) Je, taarifa za kuondolewa skuli hizo kongwe na muhimu nchini ni za kweli.

(b) Kama ni za kweli, kwa nini Skuli hizo kongwe zibomolewe kwa ajili ya ujenzi wa maduka ya biashara ambayo yanaweza kujengwa pahala pengine nje ya Mji, kipi kina thamani kubwa kati ya elimu na maduka ya biashara.

Serikali imepima vipi hasara na faida ya kuzibomoa skuli hizo, pamoja na ujenzi wa maduka hayo ukizingatia kuwa Skuli hizo zinapunguza masafa ya kufata elimu kwa vijana wetu, aidha ujenzi wa maduka hayo makubwa unazingatiaje miundombinu ya Mji Mkongwe, Msongamano wa gari, uwepo wa maegesho ya kutosha na hadhi ya Mji Mkongwe.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ: Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kabla ya kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake Nam. 156 lenye vifungu (a) na (b) kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Naibu Spika, naomba nikiri kwamba serikali inao mpango mkubwa wa kuyaendeleza maeneo mbali mbali ya mji ili kuweka haiba nzuri yenye kuvutia kwa wageni na wenyeji. Eneo la Biashara la Darajani *(Darajani Corridor)* ni mojawapo ya maeneo yaliyomo katika mpango huu. Aidha, nikiri pia kwamba baadhi ya miji duniani huendeleza maeneo yaliyo nje ya mji kwa shughuli za biashara kama ilivyotolewa mifano na Mhe. Mwakilishi.

Eneo la Darajani ni eneo muhimu kwa maisha ya kila siku kwa Wazanzibari walio wengi pamoja na wageni waliofika katika eneo hilo. Umuhimu wake unatokana na historia, utamaduni, shughuli za kijamii, kiuchumi nk. Kwa kutambua hilo, serikali imeona ni busara eneo hili likaendelezwa ili tija kubwa zaidi ziweze kupatikana. Uendelezaji huu utafanywa kwa kuzingatia yale yote yaliyolifanya eneo hili kuwa muhimu Kitaifa na Kimataifa. Bila shaka, maendeleo yoyote yanapokuja yanakuwa na changamoto zake, hivyo ni wajibu wetu kupima na kuamua juu ya faida na hasara za maendeleo hayo. Kwa mantiki hii, hata uendelezaji huu unaweza kuwa na changamoto zake hasa zile zinazotokana na mazoea. Hata hivyo, ni imani yangu kuwa mpango huu wa serikali utakuwa na manufaa zaidi kuliko hasara.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kutoa maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, katika kuliendeleza eneo la Darajani mabadiliko kadhaa yatafanywa ili kukidhi matakwa ya mpango unaokusudiwa. Ni kweli kwamba Skuli ya Vikokotoni inakusudiwa kuondoshwa na kujengwa majengo mengine ya kibiashara. Aidha, Skuli ya Darajani itathaminishwa na majengo yake yatatumika kwa matumizi mengine yatakayoendana na uendelezaji wa eneo hili.

Mhe. Naibu Spika naomba niseme wazi kabisa kwamba, kwa vigezo vyovyote vile, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inafahamu umuhimu wa elimu pamoja na dhima iliyonayo katika kutoa elimu hiyo. Hivyo basi, uamuzi wa kuzihamisha Skuli za Vikokotoni na Darajani unafanywa kwa mazingatio makubwa na kwamba utafanywa sambamba na mpango mbadala ambao utahakikisha watoto wetu waliokuwepo skuli hizo wanaendelea kupatiwa elimu inavyostahiki na bila ya kusita.

(b) Mhe. Spika, swali kwa nini Skuli hizo zibomolewe tayari nimelijibu katika kifungu (a). Aidha, katika maelezo yangu ya utangulizi nimeeleza azma ya Serikali ya kuliendeleza eneo hilo.

Kuhusu ujenzi wa maduka hayo makubwa unazingatiaje miundombinu na Mji Mkongwe, msongamano wa gari, uwepo wa maegesho ya kutosha na hadhi ya Mji Mkongwe. Maelezo yake ni kama ifuatavyo; Wazo la kuliendeleza eneo la Ukanda wa Biashara wa Darajani sio wazo geni, suala hili limekuwa likijadiliwa katika vikao vya juu vya Serikali tokea miaka iliyopita na limekuwa likitolewa maelekezo katika kila hatua ili utekelezaji wake uweze kuepuka hasara na madhara kwa kadiri inavyowezekana.

Mhe. Spika, moja ya maelekezo ya Serikali ni kwamba utekelezaji wa mpango huu uwe shirikishi, kwa maana ya kuzishirikisha sekta zote muhimu ili hoja za kisera na sheria mbalimbali zikiwemo za Mipango Miji, Mazingira, Usanifu, Uhifadhi, Usalama na kadhalika ziweze kuzingatiwa tokea hatua za awali za mpango. Hivyo basi, mambo yote muhimu na ya kitaalamu yanayohitaji mazingatio katika mpango huu, yanaratibiwa na Kamati ya Wataalamu iliyoundwa kuratibu uendelezaji wa Ukanda wa Biashara wa Darajani.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kabla ya kuuliza swali la nyongeza naomba uniruhusu nusu dakika tu nichukuwe fursa hii kuwapongeza *TANESCO* kwa kupeleka mapendekezo yao ili kuongeza bei ya umeme kwa *EWURA* ambayo hayatamgusa mtumiaji wa kawaida, hayo yamesemwa jana na Mkurugenzi Mkuu wa *TANESCO*.

Niendelee tena kuwapongeza *TANESCO* kupeleka mapendekezo yao ya kuongeza bei ya umeme kwa *EWURA* ambayo hayatamgusa mtumiaji wa kawaida, niwapongeze sana *TANESCO*. Halafu swali hili nilitegemea mimi nitajibiwa na Wizara ya Ujenzi lakini nashangaa limekuja kujibiwa na Wizara nyengine lakini ndio Serikali iko pamoja sawa.

Nchi yoyote duniani inakuwa na mji mmoja mpaka mitatu na sote tumetembea humu ndani tumeona. Mpango wa kujenga maduka ya biashara kwa nini hamkuzingatia katika miji mipya kwa mfano Tunguu, Mombasa, Fumba, Chukwani na kwengineko. Serikali inatekeleza vipi majukumu yake katika kufuata mipango hiyo, la kwanza.

La pili Skuli ya Darajani, Skuli ya Vikokotoni ni Skuli kongwe na zimetoa viongozi bora katika nchi hii, wasomi; hifadhi ya Mji Mkongwe zinalindwa vipi na sheria za *UNESCO*.

Humu ndani tulikuwa tunatunga sheria siku zote tunasema sheria tuziheshimu za utawala, zinavunjwa sasa hivi kwa misingi gani na kuhamishwa utaratibu. Eneo lile kapewa mwekezaji gani, na lipi bora kati ya elimu na hayo maduka, hebu tufahamisheni na kuna maeneo mengi, kama Fumba,Tunguu kwa nini mwekezaji kapewa pale, tumekwenda Dubai tumeona.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, nataka nimuhakikishie Mhe. Jaku Hashim Ayoub na waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba, ujenzi wa maduka ya kisasa katika eneo la Darajani umezingatia pia kuwepo na maduka katika miji mengine iliyoanzishwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Lakini kwa sababu eneo la Darajani kwa hivi sasa ndio *centre* ya biashara kwa Zanzibar, Serikali imeona umuhimu wa kuliendeleza eneo hilo la Darajani kwa kujenga maduka ya kisasa. Suala la miji mengine nataka niwahakikishie wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Mhe. Jaku, kwamba miji yote ambayo inajengwa hivi sasa katika eneo la Tunguu mji utakaojengwa kule Kijini wa *Pennyroyal*, mji unaojengwa kule Fumba yote imezingatia kuwepo kwa maduka ya kisasa. Kwa hivyo maeneo hayo yana mpango wake na eneo la Darajani lina mpango wake kama lilivyo eneo la

Michenzani na eneo la barabara kutoka Kinazini hadi Miembeni. Kila jambo ambalo linafanywa na Serikali linafanywa kwa kuangalia mipango yake na sio kufanya tu kwa sababu ya matakwa ya mtu.

Skuli ya Darajani ni kongwe na imetoa viongozi wengi, ni kweli, Skuli ya Darajani ni kongwe na nakiri kwamba imetoa viongozi wengi. Lakini kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri kwenye majibu ya msingi kwamba Skuli ya Darajani kwa sasa imeonekana kwamba hapana utulivu wa watoto wetu kuweza kupata elimu kutokana na vurugu ya wafanyabiashara, na ndio maana Serikali iliamua kuzihamisha skuli zile pale na kuzipeleka katika eneo jengine la Rahaleo. Rahaleo patajengwa skuli za ghorofa ambazo zitawaunganisha wanafunzi wanaosoma Darajani na Vikokotoni. Serikali imezingatia suala zima la uhifadhi wa Mji Mkongwe na ndio maana kamati inayoshughulikia Darajani *Corridor* ina wataalamu wa Mji Mkongwe, ina wataalamu wa Wizara ya Ujenzi, ina wataalamu wa Mipango Miji, ina wataalamu wa Ardhi, na ina wataalamu wa Mazingira, ili kuhakikisha kwamba kila sekta inazingatiwa katika kufuata utaratibu wa uendelezaji wa eneo la Darajani.

Sasa nataka niwatoe hofu Waheshimiwa Wawakilishi kwamba jambo hilo Serikali imelizingatia na hakuna jambo ambalo tutakwenda kinyume nalo katika kufanya jambo hilo la maendeleo.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-wardy: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, mimi ningeomba kuuliza swali la ziada kwa Mhe. Waziri wa Vikosi na Idara Maalum za SMZ.

(a) Kwa kuwa skuli iko Darajani na ninazungumza kwamba wafanyabiashara wanasababisha zogo, mmefikiria vipi kuweka *sound proof glasses* katika skuli ile ili kuhakikisha kwamba wanafunzi watasoma bila kusikia zogo.

(b) Kwa kuwa mna ratiba ya kwamba wanafunzi muwahamishe, mmepanga kitu gani katika eneo lile kufanya hasa katika maeneo ya skuli na shughuli gani ambayo mumeiandaa mnataka kuifanya.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, kuhusu mpango wa kutengeneza miundombinu ambayo itawafanya wanafunzi wasiweze kusikia mazogo yaliyopo pale katika eneo la Darajani, nimuombe Mhe. Mwakilishi akumbuke katika majibu yangu kwamba sasa hivi katika mpango tulionao ni kwamba skuli itaondoka. Sasa kama skuli inaondoka nadhani niseme wazi

kwamba dhamira ya Serikali kwamba pale hakutakuwa na mpango wowote katika uendelezaji wa skuli, kwa sababu skuli ile tunatarajia kuihamisha katika eneo lile na kuipeleka eneo jengine ili pale itoke fursa ya kufanya mengine ambayo yamekusudiwa.

Vile vile kuhusu shughuli ambazo zinakusudiwa kufanywa pale nadhani katika kamati ambayo imeundwa ni kamati ambayo imeshirikisha taasisi mbali mbali na wataalamu mbali mbali wenye fani tofauti. Kwa mantiki hiyo baada ya hatua za ujenzi zitakapoanza kufanyika nadhani maelekezo mbali mbali nini kifanyike katika maeneo yale, lakini zaidi kuboresha kutakuwa shughuli mbali mbali zitafanywa au mambo yatayowekezwa pale kutakuwa na maegesho, kutakuwa na sehemu ya bustani, kutakuwa na sehemu za maduka, nadhani na mambo mengine kama hayo.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Naibu Spika, nikushukuru pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri nitauliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa dhamira ya Serikali ni njema ya kuboresha mji wetu na kujenga maduka ya kisasa na maeneo mazuri ili kuleta haiba katika nchi yetu. Lakini tangu zoezi hili limeanza ni muda mrefu na tutatarajia matunda haya yaje kwa haraka. Nilitaka kujua ni lini hasa ujenzi wa *corridor* Darajani utaanza.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi kwamba katika hatua ya ujenzi ni kwamba kuna hatua mbali mbali lazima zipitiwe kwanza na hatimaye shughuli iliyokusudiwa ianze kufanyika. Sasa hivi hatua tuliokuwanayo ni kuwa suala la michoro katika eneo lile ambalo limekusudiwa kufanya hiyo kazi tayari zimeshakuwa katika hatua za mwisho, na baada ya kumalizika hatua hiyo nadhani kutakuwa na hatua nyengine ambayo kwa kweli tunategemea sana kwamba ujenzi utaanza kutekelezwa pale endapo hatua nyengine ambazo zimeshapitiwa.

Nam. 140

Ujenzi wa Nyumba za Kurekebisha Tabia *(Sober House)* – Kidimni:

Mhe. Yussuf Hassan Iddi **-** Aliuliza

Serikali kwa nia njema inajenga kituo maalum cha kurekebisha tabia vijana walioathirika na Dawa za Kulevya katika eneo la Kidimni Wilaya ya Kati.

(a) Je, ni kiasi gani mpaka sasa kishatumika katika ujenzi huo.

(b) Ni lini kituo hicho kitakamilika.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais – Alijibu

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 140 lenye vifungu (a) na (b) naomba kutanguliza maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kabisa kwa nia njema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tumeamua kujenga Kituo cha Kurekebisha Tabia "*Rehabilitation Centre*" kwa ajili ya watu walioathirika na matumizi ya madawa ya kulevya katika eneo la Kidimni Wilaya ya Kati Unguja.

Mhe. Naibu Spika**,** pamoja na ujenzi wa kituo hicho Serikali pia imeweka utaratibu wa kusaidia nyumba binafsi kumi na mbili (12) za kurekebisha tabia *'Sober House'* zilizopo Unguja na Pemba, kila nyumba hupatiwa Shilingi milioni moja na laki tano kwa mwaka.

Mhe.Naibu Spika**,** tunawapongeza sana wale wote wanaojitolea katika kusaidia waathirika wa madawa ya kulevya. Pia tunawaomba waliopona kutokana na kuacha kutumia madawa ya kulevya wasirejee tena na wawe walimu bora kwa wenzao ambao bado wamekuwa ni waathirika wa madawa ya kulevya.

Mhe. Naibu Spika**,** naomba sasa nimjibu Mhe. Mwakilikishi wa Jimbo la Fuoni, Yussuf Hassan Iddi swali lake namba 140 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, hadi hivi sasa jumla ya Tsh. bilioni moja milioni mia nne na ishirini na nne, tisiini na tisa elfu mia moja na arubaini na tano (1,424,099,145) zimeshatumika ambazo ujenzi wake kwa hatua ya awali umeshafanyika na kuanza kutumika na waathirika.

(c) Mhe. Naibu Spika, muda wa ujenzi wa kituo hicho unatarajiwa kuwa ni wa kipindi cha miaka mitano (5) yaani 2013-2017. Mhe. Naibu Spika, Serikali imedhamiria kukamilisha ujenzi huo wa kituo hicho kwa awamu tofauti ndani ya kipindi chake cha miaka 5 ambacho ujenzi huo unategemea zaidi fedha zetu za ndani na sio wahisani.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Ahsante Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo.

Kwa kuwa katika majibu ya swali mama alisema jumla ya shilingi 1.4 bilioni zilitumika kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho, je, jengo lililokuwepo sasa hivi linalingana na thamani ya fedha zilizotumika yaani *value for money* na kama hailingani na thamani iliyotumika.

(b) Serikali imechukua hatua gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, tukubaliane na ndugu Mjumbe kwamba ni kweli jengo lile kama ambavyo tumejibu katika jibu letu la msingi kwa hatua ya awali ujenzi umekamilika, lakini tukitizama inawezekana uhalisia *value for money* inawezekana ikawa ni vitu ambavyo haviendi sambamba. Na sisi kama Wizara kwa kuliona hilo na kulitambua, hilo tumeshaliona na tumeendelea na mchakato wa ndani wa kuhakikisha kilichofanyika pale kinaendana na matumizi ya hali halisi ya ile fedha ambayo imetoka.

La pili Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mjumbe ameuliza Serikali imechukua hatua gani, tukubaliane naye kwamba dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kila kinachotoka kinatumiwa katika misingi iliyokuwa bora zaidi. Tunachokifanya kwa hatua za awali ni kufanya utafiti kutizama dosari ilitokea wapi ili itakapokuja kuthibitika na kubainika ndio pale sasa Serikali itakuja kuchukua hatua za kiutendaji zaidi.

Mhe. Hamida Abdalla Issa: Ahsante Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri na mimi ningependa kumuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa madawa hayo yanayowaathiri vijana tunaamini hayatengenezwi hapa katika nchi yetu ya Tanzania na Visiwa vyetu vya Zanzibar kwa ujumla. Napenda nimuulize Mhe. Naibu Waziri, je, ni watu wangapi ambao wamewahi kushikiliwa kwa uingizaji wa madawa hayo na ni hukumu gani ambayo wamepatiwa. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, ni vigumu kusema ni watu ambao wameshathibitika ama kukamatwa na madawa ya kulevya. Ingawa Serikali inatambua zipo baadhi ya kesi na yapo baadhi ya mashauri yapo katika ngazi husika za mahkama ama vyombo mbali

mbali ambavyo kuna baadhi ya kesi ushahidi wake haujakamilika, hukumu zitakapokuja kutoka, Serikali ndio itatambua na kujua rasmi sasa idadi ya waliokamatwa na kuthibitika. Lakini pia itajua idadi ya *suspicious* wa madawa ya kulevya na Serikali inatambua kwamba waathirika wakubwa wa janga hili ni vijana. Ahsante sana.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, amesema kwamba kuna nyumba za kulelea vijana hawa Unguja na Pemba. Lakini nataka nimuulize swali dogo tu, Mhe. Naibu Waziri kila kukicha vijana hawa wa madawa ya kulevya wanaongezeka mitaani na kusambaa, je, ni hukumu gani zinazochukuliwa kama kupigwa bakora au ni hukumu gani zinazochukuliwa kama kupigwa bakora au ni hukumu zinazochukuliwa nyengine kuwadhibiti vijana hawa wasiongezeke.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, ni kweli asilimia kubwa ya watu ambao wanaathirika na madawa ya kulevya ni kundi kubwa sana la vijana. Serikali imeliona hilo, lakini taasisi na idara tofauti za nchi hii pia zimeweza kulitambua hilo. Dhamira kubwa ya serikali ambayo imeamua kufanya katika jambo hili, kwanza ni kutizama mianya yote ya uingizwaji wa dawa za kulevya vipi tunaweza kudhibiti. Jitihada mbali mbali zimeanza kuchukuliwa, lakini pia tujue kuna mikakati maalum ya ndani ambayo si vyema kuweza kuizungumza katika maeneo yote, kwa dhamira ya kuweka mitego ili kuweza kuwapata watu ambao wanajihusisha na biashara hii haramu ya madawa ya kulevya.

Nam. 126

Nyongeza ya Mishahara kwa Wafanyakazi wa SMZ

Mhe. Suleiman Sarahan Said – Aliuliza:-

Zanzibar ina wafanyakazi wachache wa serikali ukilinganisha na wafanyakazi wa Serikali ya Jamuhuri ya Muungano. Wafanyakazi hawa wakifanya kazi kwa pamoja, wafanyakazi wa Serikali ya Zanzibar na ile ya Jamhuri ya Muungano hupelekea wafanyakazi wanaotoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar huona kuna uonevu fulani, kwa kuwa kuna tofauti kubwa ya mishahara ambapo kwa wafanyakazi wa SMZ maslahi yao ni madogo sana.

(a) Je, serikali haioni umuhimu wa kupandisha kima cha mshahara angalau kuendana na wenzao.

(b) Je, ni tatizo gani ambalo linafanya mishahara ya wafanyakazi wa Zanzibar ikawa midogo sana.

(c) Je, lini serikali itaweza kufikia lengo hilo la kupandisha mishahara ili kwenda na kasi ya kupanda kwa gharama za maisha.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mheshimiwa swali lake lenye nambari 126 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi, naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mhe. Naibu Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kama ilivyo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na serikali nyengine ulimwenguni inawathamini na kuwafikiria sana watumishi wake kimaslahi.

Mhe.Naibu Spika, katika huthibitisha hilo, nadhani itakumbukwa kwamba ndani ya kipindi cha uongozi huu wa Awamu ya Saba wa Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein, serikali imepandisha kima cha chini cha mshahara mara mbili. Kwanza kwa asilimia 25, kutoka Shs. 100,000/= hadi Shs 125,000/= kwa mwezi mwaka 2011 na kwa asilimia 20 kutoka Shs 125,000/- hadi Shs. 150,000/= kwa mwezi mnamo mwaka 2013. Marekebisho pia yamefanywa kwa mishahara ya watumishi wengine wote wa umma.

Mhe. Naibu Spika, mbali na marekebisho haya, serikali pia ilipanga upya ngazi za mishahara ya watumishi kuwapatia nyongeza maalum watumishi wa muda mrefu, kurekebisha maposho mbali mbali na mishahara ya wataalamu kwa mujibu wa kada zao ili kupunguza wimbi la wataalamu hao kuhama katika Utumishi wa Umma na kwenda kufanya kazi kwengineko. Hizi ni baadhi tu, ya hatua zilizolenga kuongeza maslahi ya watumishi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kuyafanya yawe bora.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Naibu Spika, serikali tayari imekwishaamua kupandisha kima cha chini cha mshahara ifikapo mwezi wa Aprili, 2017 kutoka kima cha sasa cha Shs. 150,000/- na kufikia kima cha chini cha mshahara cha Shs. 300,000/=

kwa watumishi wake. Kwa kiasi fulani kima hiki cha mshahara kitaendana na kile kinacholipwa kwa watumishi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

b) Mhe. Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika maelezo yangu ya utangulizi, Serikai ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Awamu ya Saba imefanya marekebisho ya mishahara kutoka Shs 100,000/= hadi Shs 150,000/= na kuongeza maposho mbali mbali katika kipindi cha 2011 na 2014. Hatua hizo ni miongoni mwa jitihada zinazochukuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuimarisha maslahi ya watumishi wake.

Mhe. Naibu Spika, kwa ujumla mishahara ya watumishi katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar sio midogo ikilinganishwa na mishahara wanayolipwa watumishi wengine katika nchi mbali mbali za ukanda wa Afrika Mashariki. Kinachofanyika hivi sasa ni kuinua kima cha chini cha mshahara ili nacho kiwe cha kuridhisha. Hata hivyo, uzoefu unaonyesha katika nchi nyingi duniani suala la ulipaji mishahara linategemea sana uwezo wa serikali.

c) Mhe. Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika jawabu (a), Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imepanga kufanya marekebisho ya mishahara ifikapo Aprili, 2017 ili kuendana na gharama za maisha. Serikali itaendelea kuchukuwa hatua za kupandisha mishahara kulingana na hali ya maisha ilivyo kila hali ya uchumi wa nchi yetu itakapokuwa nzuri. Ahsante.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana, kwanza nimpongeze Mhe. Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri. Pia, nimshukuru Rais Dkt. Ali Mohammed Shein kwa kupandisha mishahara kwa asilimia mia moja kwa kima cha chini, hili lazima nimpongeze sana.

Mhe. Naibu Spika, lakini nilikuwa nina swali la nyongeza, kwamba kuna taarifa tu kuwa kuna badhi ya idara huwa wanapokwenda kwenye semina zao au mambo mengine Bara huwa wanalipana vizuri na wengine huwa hawalipani vizuri. Sijui suala hili kwanza ni kweli au si kweli, lakini hilo ni swali la kwanza.

Pili, nilikuwa nazungumzia kwamba, kama suala la mishahara limekaa vizuri basi kuna suala ambalo kuwa tuna watu wetu au idara zetu zinafanya kazi kwa pamoja na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Je, hatuoni umuhimu ule wakati wa kufanya kazi kwa pamoja tukakidhi haja ya wale wenzetu kwa vigezo vyote ambavyo wenzetu wanapewa.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, suala la baadhi ya idara za serikali kulipana mafao mazuri wanapohudhuria vikao mbali mbali katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania taarifa hii sisi bado hatujaipokea. Lakini kama hali hii ipo naomba Mhe. Mwakilishi tuweze kushirikiana kuhakikisha kwamba tunapata ukweli wa jambo hili na zile hatua ambazo tunaweza kuchukua tuchukue ili kutatua tatizo hili. Kwa hivyo, naomba sana Mhe. Mwakilishi, tushirikiane kwa hili kama lipo tuweze kulitatua kwa ushirikiano wako kwa pamoja.

Pili, kuhusiana na suala la wafanyakazi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kufanya kazi pamoja kwa mashirikiano ya karibu na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kufikia lile lengo la uboreshaji wa maslahi. Naomba kujibu kwamba, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inafanya kazi kwa karibu sana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa upande wetu wizara huwa tunakutana kila baada ya muda fulani na wizara inayohusika na masuala ya utumishi kule Tanzania Bara. Kwa hiyo, tunapokutana katika vikao vyetu hivi huwa tunabadilishana mawazo kwa mambo mbali mbali ili kuhakikisha kwamba wafanyakazi wetu wote wa pande zote mbili za nchi yetu wanaweza kufaidika katika yale maslahi yao ambayo wanapaswa kufaidika nayo. Lakini kubwa zaidi tunachokiangalia ni kwamba sheria yetu inasemaje, kanuni zetu zinasemaje, hapo ndipo tunapofanya maamuzi pamoja na kwamba tunakuwa tunashirikiana nao kwa ukaribu zaidi.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana na mimi kunipa nafasi. Kwanza nimpongeze Mhe. Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri hasa kwenye suala hili la nyongeza ya mishahara.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

(a) Wizara yake inafahamu kwamba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali wako wafanyakazi ambao walikuwa wanastahiki kupata nyogeza lakini mpaka leo hawajapata nyongeza hiyo.

(b) Ni lini serikali itaweza kuwapatia nyongeza hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, naomba nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kwamba, kuna baadhi ya wafanyakazi wa serikali na sio Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali tu, pia na wizara nyengine kwamba katika ule urekebishaji

wa maslahi uliopita kuna baadhi ya wafanyakazi marekebisho yale hayakuwa sawa. Kwa maana hiyo, suala hilo tunalijua na tayari tumekuwa tukilifanyia kazi siku hadi siku kuhakikisha kwamba wale ambao stahiki zao wanapaswa kuzipata kama wanavyozipata wale wenzao basi stahiki hizo waweze kuzipata.

Swali lake la (b). Mhe. Naibu Spika, Mheshimiwa, ametaka kujua kwamba ni lini maslahi yao haya yatakaa sawa? Tunategemea kabla ya mwezi Aprili, 2017 baada ya hii mishahara mipya kutoka, suala hili liwe limeshakamilika. Kwa sababu tukienda nalo mpaka mshahara huu unaokuja wa Aprili kutakuwa kuna mazonge zaidi, lakini tunahakikisha kwamba kabla ya kufika Aprili, 2017 mishahara mipya kuanza suala hili tuhakikishe kwamba tunalimaliza na wale wote wanaostahiki kupata haki zao kulingana na Sheria ya Utumishi pamoja na kanuni zetu za utumishi wa umma wanapata maslahi yao kama wanavyopata maslahi wale wafanyakazi wengine.

Nam. 97

Uimarishaji wa Makumbusho ya Mkamandume Pemba

Mhe. Ali Khamis Bakari - Aliuliza:-
Serikali kwa kuthamini uchumi na kuimarisha utalii imeona kuimarisha Sekta ya Utalii. Hivyo, kuna majengo ya makumbusho ya kale Chwaka, Tumbe (Msikiti Chooko) kama vile Mkamandume, Pujini Kisiwani Pemba yametupwa jambo ambalo linaweza kuingiza fedha kupitia sekta hii na kuyafanya majengo haya yatambulikane rasmi.

(a) Je, wizara ina mpango gani wa kuyaimarisha makumbusho yale ili wananchi wasiendelee kuyaharibu na kuyafungia wanyama.

(b) Vipi wananchi wa Jimbo la Tumbe watafaidika na ajira pale ambapo makumbusho yake yatafanya kazi.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo - Alijibu:-

Mhe.Naibu Spika, kwa idhini yako kabla ya kumjibu Mheshimiwa swali lake Nam. 97, naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, wizara inakubaliana na mawazo ya suala hili ambapo katika juhudi za kukuza uchumi ipo haja ya serikali kuimarisha sekta ya utalii kwa kuimarisha majengo ya kihistoria.

Mhe. Naibu Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa kwamba, majengo ya Makumbusho ya kale ya Chwaka, Tumbe (Msikiti Chooko) na yale ya Mkamandume yalioko Pujini Kisiwani Pemba yapo katika hali isiyokuwa nzuri, lakini hayajatupwa kwa vile yanatambuliwa kihistoria kwa mujibu wa sheria za hifadhi.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo kwa ruhusa yako sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 97 kama ifuatavyo:-

(a) Katika kuimarishaji maeneo hayo ili wananchi wasiendelee kuyaharibu na kuyafungia wanyama, serikali kupitia idara yake ya Makumbusho na Mambo ya Kale inaendelea kuchukua juhudi za kuimarisha ulinzi kwa kuziimarisha kamati za uhifadhi katika maeneo yote mawili. Pia, hatua za kuapatia hati miliki zinaendelea kusimamiwa.

(b) Makumbusho hayo baada ya kuimarishwa na yatakapoanza kufanya kazi wananchi wa Jimbo la Tumbe watashirikishwa moja kwa moja katika ajira na uhifadhi na uimarishaji wa maeneo hayo. Ajira za wafanyakazi katika maeneo hayo zitatokana na vikundi vya uhifadhi katika eneo hilo, lakini pia makusanyo yatakayopatikana yatatumika katika kuchangia maendeleo ya Sekta ya Utalii na Shehia husika. Ahsante.

Mhe. Ali Khamis Bakari: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, napenda kumuuliza swali jengine la nyongeza. Kwa kuwa makumbusho haya yamekaa kwa muda mrefu ni lini sasa yatafanya kazi zake kama inavyotakiwa. Wafanyakazi wangapi wanahitajika kupatikana pale au kupelekwa kufanya kazi pale.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, kama nilivyojibu katika jibu mama, makumbusho haya pale ambapo yatamalizika tu kiutaratibu wake na kuanza kufanya kazi yataendelea kufanyakazi na wafanyakazi ambao wataajiriwa katika sehemu ile husika itategemea na mahitaji ambayo yatakuwepo katika sehemu ile.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, makumbusho ni historia iliyopita na vizazi na wengineo hutegemea kujua ilivyoanzia na inavyoendelea.

Mhe. Naibu Spika, kwa wenzetu nchi za nje ukienda kama Msumbiji siku iliyoanza risasi ya kugomboa nchi yao bunduki au mzinga ule umewekwa katika kumbukumbu. Je, kwa kuwa hiyo ni kumbukumu ya historia ya nchi yao na watalii wanakwenda kutembea pale, yale magofu yetu kama ya Mkamandume ambapo limebakia eneo tupu halina kitu. Wizara ina mpango gani wa kutafuta wawekezaji ambao waingie ubia na Kamisheni ya Utalii au serikali kuweka eneo lile ujenzi ule uwepo ili kuleta faraja kwa watalii wanapokwenda kule waone kitu badala ya kuona lile eneo tupu.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, kwanza nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba, katika sehemu za utalii yakiwemo maeneo yetu ya historia ni sehemu muhimu sana kwa historiaya nchi husika.

Naomba nimwambie Mwakilishi kwamba, wizara katika sehemu hii imepanga na sasa hivi na tayari imeshaandaa Programu za kuwatafuta wafadhili kwa kuwa haya maeneo tayari yameonekana yameshaanza kupoteza ule uhalisia wake imeandaa mpango wa kuwatafuta wafadhili ili kuyahifadhi maeneo yale na kuyarejesha katika historia yake. (*Makofi*)

UTARATIBU

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Naibu Spika, nasimama kwa kutumia Kanuni ya 37(1), ambayo inawesema:

"Waziri au Mjumbe yeyote anaeuliza swali ambalo ana madaraka nalo atakuwa na wajibu wa kujibu swali hilo kwa ukamilifu kwa usahihi na kwa ufupi, isipokuwa kwamba swali alilouliza waziri mmoja linaweza kujibiwa na waziri mwengine au Mwanasheria Mkuu"

Mhe. Naibu Spika, swali alilouliza Mhe. Mwakilishi, aliuliza ni kwamba, je, kuna mpango gani serikali kuingia ubia ili kuweza kulinda haya maeneo na kuyaendeleza.

Mhe. Naibu Waziri, alipokuwa akijibu swali, ametamka kwamba kutafuta wafadhili ni vitu viwili tafauti, ubia na kutafuta wafadhili. Ahsante.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri, naomba ujibu sahihi.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Nashukuru sana Mhe. Naibu Spika, na nataka kumpongeza sana Mhe. Naibu Waziri wa Habari,

Utalii, Utamaduni na Michezo, kwa kujibu suala kwa ufasaha na usahihi kwa mujibu wa alivyolifahamu.

Hata mimi Mhe. Naibu Spika, nimemfahamu muulizaji Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata), ameuliza ni vipi wizara imejipanga katika kuwatafuta wafadhili watakaoweza kuyajenga majengo yale na kuhakikisha kuyarudisha kwenye historia yake kama ilivyo awali. Njia ya kupata wafadhili ndio njia pekee ya kuingia ubia namna ya kuyajenga yale majengo ya historia.

Kwa hivyo, kwa mujibu alivyoeleza Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo, ni kwamba wizara imejipanga na imeweka Programu zake za kutafuta wafadhili ambao wanaweza kusaidia kuyarejesha majengo yale katika haiba yake na wafadhili hao wanaweza kuwa kwa njia ya ubia, wanaweza kuwa kwa njia yan kujitolea au wanaweza kufanya ile kazi kwa njia ya ku-*build, operate and transfer*, wakayatumia na baadae wakaweza kuyarudisha kwa serikali.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, nashukuru sana kwa majibu yaliyotolewa na namshukuru sana Mhe. Simai Mohammed Said, kwa ufafanuzi alioutoa. Lakini ubia wake aliouona utapatikana utapatikana baada ya kupata hao wafadhili ndipo tutaendelea na mpango wa kuingia ubia na mfumo wa kujenga hayo majengo. Nashukuru sana Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

Mhe. Maryam Thani Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja ya nyongeza.

Katika sehemu zote ambazo kunahifadhi au taasisi za serikali kunakuwa na walinzi. Je, katika sehemu zote za Magofu ya Makumbusho walinzi wake wanapatikanaje ukizingatia kwamba wananchi wanafanya uharibifu katika sehemu hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Naibu Spika, naomba niwambie Mhe. Maryam Thani Juma, kwamba nakiri kwamba katika taasisi zetu zote za serikali na za binafsi zinakuwa na ulinzi. Katika wizara yetu walinzi katika sehemu hizi za histori wapo walinzi ambao tumewaajiri moja kwa moja kutoka serikalini na kuna walinzi tuliowaajiri kupitia katika vikundi vyetu vya hifadhi katika sehemu husika. Ahsante.

Nam.153

Kuongezeka kwa Ajira katika Sekta ya Utalii:

Mhe. Viwe Khamis Abdallah (Kny; Mhe. Tatu Mohamed Ussi): Aliuliza:- Sekta ya Utalii inaaminika kwamba ni moja kati ya sekta muhimu zinazochangia kwa kiasi kikubwa katika uchumi wa nchi yetu pamoja na kutoa ajira kwa vijana wetu.

(a) Vijana wangapi wameajiriwa katika sekta hii ya utalii na kwa kiasi gani imepunguza wimbi la vijana wasiokuwa na ajira.

(b) Ni kwa kiasi gani Sera ya Utalii kwa wote imetekelezwa tangu kuanzishwa kwake.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo - Alijibu:- Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako napenda kumjibu Mhe. Tatu Mohamed Ussi, swali lake 153 lenye vipengele (a) na (b).

Kabla ya kumjibu swali lake Mhe. Mwakilishi, naomba kutoa maelezo kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, Kwanza kabisa napenda kukiri kuwa sekta ya utalii ni miongoni mwa sekta muhimu zinazochangia kwa kiasi kikubwa katika uchumi wetu na asilimia 80 ya fedha za kigeni Pamoja na kiasi kikubwa cha kutoa ajira kwa vijana wetu na kwa jamii. Aidha, sekta ya utalii hujumuisha sekta ndogo ndogo zikiwemo huduma za malazi na chakula, usafirishaji kwa njia ya Anga, bahari, maji, barabara, michezo, utoaji wa taarifa, utamaduni na historia ya nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, nichukuwe fursa hii pia kuwakumbusha Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein, kwa makusudi aliasisi falsafa ya "Utalii kwa Wote" mwaka 2010. Malengo makubwa ya kuanzishwa na kutekelezwa kwa falsafa hiyo ni kuhakikisha kuwa sekta ya utalii kwa wote unaleta manufaa na tija kwa wananchi wa rika na jinsia tofauti na katika maeneo yote ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kutoa maelezo hayo mafupi, naomba uniruhusu kujibu suali la Mhe. Tatu Mohamed Ussi. lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, Sekta ya utalii kwa ujumla wake inakadiriwa kuajiri jumla ya wafanyakazi wa rika mbali mbali wapatao takribani 22,000 ambapo asilimia 73 ya ajira hizo zimetolewa kwa vijana. Hii inamaanisha kuwa jumla ya vijana 16,060 wameajiriwa kutoa huduma katika sekta ya utalii ikiwemo huduma za malazi, huduma za usafirishaji kwa njia ya barabara, bahari na anga, huduma za kutembeza na kutoa taarifa kwa wageni na kadhalika.

(b) Mhe. Naibu Spika, Tokea kuasisiwa kwa falsafa ya 'Utalii kwa Wote' na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Serikali imechukuwa hatua mbali mbali ili kufikia azma ya falsafa hiyo. Miongoni mwa hatua zilizochukuliwa ni kama zifuatazo:-

Kwanza, kuitambua falsafa hiyo kwa misingi ya kisheria.

Pili, kuunda kamati za utalii za wilaya kwa lengo la kuteremsha shughuli za utalii katika ngazi za wilaya.

Tatu, kushajihisha wananchi kwa kuanzisha vikundi vya ushirika ambavyo vitatoa huduma kwa sekta ya utalii.

Nne, kuandaa programu mbali mbali kwa ajili ya kuwashajihisha wananchi umuhimu wa kutembelea maeneo ya kitalii.

Tano, kuzishirikisha taasisi mbali mbali za umma na binafsi katika ujenzi wa miundombinu ya utalii ikiwemo maji, ulinzi, umeme na barabara.

Sita, kuzishirikisha taasisi mbali mbali za umma na binafsi katika harakati za kutangaza bidhaa na huduma za utalii zilizopo Zanzibar. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Viwe Khamis Abdallah: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa utalii umekuwa zaidi kwenye maeneo ya vijijini.Je, Mhe.Waziri, wananchi hawa ambao wapo katika maeneo hayo ya utalii wanafaidikaje na utalii huo.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Naibu Spika, naomba niwambie Mhe. Mwakilishi kwamba katika sekta hii vijana

wetu wanafaidika na faida mbali mbali moja wapo ni kupatiwa ajira vijana wetu katika sekta hii ya utalii. Ahsante Mhe. Naibu Spika. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Naibu Spika, Mhe. Naibu Waziri, hongera kwanza kwa majibu mazuri, marefu, lakini ningeomba nikuulize swali dogo la nyongeza. Kama Wizara huwa mnatoa mashirikiano gani na wanavijiji wahusika ambao wamekabiliwa na lile suala la utalii ndani ya kijiji chao. Vijana huwa mnawapa mashirikiano gani ili kuweza kupata ajira kutokana na zile changamoto zao za kimaisha.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Naibu Spika, kupitia sekta ya utalii kwa vijana, wizara inashirikiana nao kwa kuwashirikisha katika sekta hii, kwa mfano sasa hivi tumeanzisha Programu maalum kwamba wale vijana ambao wanashughulika katika sekta hii kwa mfano kutembeza wageni lazima wapitie katika sekta yetu ya utalii na vijana wale kuhakikiwa ili shughuli hizi wasifanye wageni. Ahsante. Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa sekta hii ya utalii ni moja katika vianzio vyetu muhimu na kwa sababu sekta hii ya utalii kwa kisiwa cha Pemba utekelezaji wake bado ni wa kusuasua ukilinganisha na upande wa Unguja kutokana na changamoto mbali mbali zinazozikabili.

(a) Je, serikali ina mpango gani wa makusudi wa kuwapa msamaha maalum kwa wale wawekezaji ambao wana nia thabiti ya kuekeza kule Pemba.

(b) Je, serikali haioni kwamba kukosa kuwapa ule msaada maalum wale wawekezaji wa huo msamaha unaweza kusababisha wawekezaji hao kuondoka na kuikosesha serikali mapato madogo ambayo kwa sasa tunayapata na kusababisha serikali kukosa hayo mapato. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo:

(a) Mhe. Naibu Spika, suala zima la msamaha linafuata sheria, taratibu na kanuni za utalii pamoja na kanuni na sheria na taratibu za kodi.

Hivyo, suala la kuweka upendeleo maalum kwa wawekezaji maalum halitakuwa na tija katika kukuza utalii. Kilichokuwepo kwa wawekezaji wetu na waliokuwa tayari kuwekeza kule Pemba basi ni kufuata zile taratibu ambazo zipo na misamaha ipo wafike katika vile vituo vyetu vya *ZIPA* na vitu vile vya utalii watajua misamaha inayotolewa na inayopatikana.

(b) Kusema kwamba kutokutolewa msaada au msamaha wa aina hii kunakosesha mapato madogo madogo. Nataka nimthibitishie kwamba utalii Pemba umekuwa vizuri na hivi sasa mapato yanayokusanywa Pemba wamekuwa ni makubwa ukilinganisha na muda wote uliopita hapo nyuma na utalii Pemba ndio sehemu ambayo ina vivutio vizuri hususan kwa upande wa bahari na kwa upande wa mahoteli. Hivyo, endapo wawekezaji watatumia fursa hii vizuri naamini utalii kwa Pemba utakuwa zaidi na fursa zipo na wao wanaweza kuweka mchango mkubwa katika mapato ya serikali. Nashukuru sana Mhe. Naibu Spika.

Nam 47

Ukosefu wa Umeme Skuli ya Msingi ya Ungi Msuka

(Mheshimiwa Mjumbe aliyetaka kuuliza swali hili ameliondoa)

Nam. 50

Kuhamasisha Wananchi Matumizi ya Umeme:

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza:-
Serikali inafanya juhudi kubwa ya kuwasogezea huduma ya umeme wananchi, lakini baadhi ya sehemu hautumiki kabisa na pengine kupata hasara.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuhamasisha wananchi kutumia umeme zaidi ili ataetumia umeme sana apunguziwe na kupewa punguzo kwa utumiaji zaidi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 50 kama ifuatavyo:

Lengo la Serikali ni kuwa kila mwananchi apate huduma hii ya umeme. Ili kufikia lengo hilo, Shirika la Umeme limekuwa na utaratibu wa kuwashajihisha wananchi kuunga umeme na kuutumia kwa uwadilifu. Vile vile, Shirika

limeweka utaratibu wa kutoa fursa ya uungaji wa umeme kwa njia ya mkopo kwa yule ambaye hana uwezo wa kulipia gharama za uungaji kwa pamoja.

Katika kuhamasisha uungaji wa umeme, Shirika limekuwa na utaratibu wa kutoa elimu juu ya umuhimu wa kutumia fursa iliyotolewa na serikali ya kuunga umeme kwa mkopo na kipaumbele zaidi kimewekwa kwa wananchi wa vijijini pamoja na wenye kipato kidogo. Ahsante sana.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Ahsante Mhe. Naibu Spika, pamoja na kushajihisha katika mazingira ambayo unaweza kuchukuwa lugha moja husema; "Mcheza kwao hutunzwa"

(a) Je, Mhe. Waziri, kwa wale watu ambao wa marika ya kati au katika utumiaji wa kati au wa chini ambao wanatumia umeme zaidi katika kujihamasisha. Je, wanautaratibu au wamewawekea japo *bonus* fulani ili kutia moyo kwa wengine wanaotumia.

(b) Mpaka sasa hivi ana udhibiti gani au ana kauli gani ya kuzungumza kwamba Shirika lake la Umeme, umeme wake unaoibiwa una kima cha kiasi gani unaoibiwa na watu wasiipendelea Zanzibar maendeleo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira:

(a) Mhe. Naibu Spika, tunaenda kwa usawa, yaani utalipa kwa kadri unavyotumia.

(b) Tunaendelea na kubai hawa wezi, ama wahalifu, ama wasiotutakia mema na kadri hali itakavyokuwa wanapatikanwa na taarifa zinakuwa zinatolea.

Lakini pia niombe Waheshimiwa Wawakilishi kwa ujumla tusaidiane katika hili kwa sababu hawa athari yake ni kwa taifa zima na sio tu kwa yule ambaye tunamuona kwamba shirika mwenye dhamana ya kufanya hivyo. Kwa sasa kwa takwimu wangapi labda tumewakamata sinazo ila nitakupatia *Inshaallah* kwa maandishi.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi ninashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza swala dogo la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba nimuulize swali dogo la nyongeza.

Umeme ni umuhimu sana kwa maisha ya binaadamu kwa kila siku. Kule Ndagoni kuna kijiji kinaitwa Ngagu Mkumbuu na umeme ndiko ulikotoka, hadi hivi sasa wananchi wale bado hawajapata umeme. Je, ni lini Shirika hili la Umeme litawafikishia umeme kule.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Ardhi: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Ni kwamba tumelipokea na tutalifanyia kazi. Ahsante sana.

Mhe. Maryam Thani Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kunipa fursa hii.

Kwa kuwa azma ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kufikisha umeme katika vijiji vyote vya Zanzibar na kauli ya Mhe. Rais wa Zanzibar, alisema kwamba katika Kisiwa hichi cha Fundo kitafikishiwa umeme na sasa hivi hatua zinaanza. Je, ni hatua gani iliyofikiwa ya kufikishiwa umeme katika Kisiwa hichi cha Fundo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Ardhi: Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Ni kweli kwamba Shirika ama Serikali ina azma ya kuwafikishia umeme wananchi, lakini naomba niseme jambo kwamba, tuna tofauti kati ya vijiji, tujue kwamba si kila nyumba mbili zimejengwa leo kuwa itakuwa tafsiri halisi ya kijiji. Na hii isije ikachukuliwa hoja kwamba mbona kijiji fulani hakijapata umeme.

Ahadi ya Serikali ni kwamba mpaka kufikia mwaka 2020 vijiji vyote vimepata umeme. Lakini isije ikachukuliwa nyumba mbili zimejengwa leo kwamba kwa nini kijiji hichi hakijipata umeme.

Lakini Mhe. Naibu Spika, nikija katika suala la Kisiwa cha Fundo ni kwamba, hatua zinaendelea na Kamati ya Mawasiliano ilishuhudia tulifika katika eneo ambalo utasafirishwa umeme upelekwe kule Kisiwani Fundo. Jitihada zinaendelea. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Ardhi: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba niongezee tu baada ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wangu aliyoyatoa, nilikuwa na karatasi mkononi Kisiwa cha Fundo sasa hivi kuanzia mwezi unaofuata wa Disemba basi katika kisiwa hicho cha Fundo kazi ya kupeleka nguzo utaanza. Na utaratibu tayari umeshachukuliwa na sasa hivi ndiyo iliyokuwa inathibitisha kuanza kazi mara moja. Kwa hivyo, naomba kumuarifu Mhe. Mwakilishi, kwamba usiwe na wasi wasi hatua zinachukuliwa. (*Makofi*)

Nam. 54

Kuwepo kwa Eneo la kupumzikia katika Mji wa Chake Chake

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza:-

Katika eneo la ufukwe wa Tibirinzi zamani maeneo hayo yalikuwa yakitumiwa na wazee na vijana kwa kujipumzishia na kuogelea, sasa maeneo hayo yamefukiwa na mikoko na Chake Chake ni Mji wa Pili kwa Zanzibar na haina sehemu nyengine ya kupumzikia na kuogelea.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwa na sehemu kama hiyo katika mji huo wa Chake Chake.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira – Alijibu:-
Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suala lako namba 54 kama ifuatavyo:-
Kabla ya kujibu suala la Mhe. Mwakilishi, napenda kutoa maelezo mafupi yafuatayo:

Serikali inatambua kuwa Chake Chake ndio mji wa pili kwa Zanzibar na pia inaona umuhimu mkubwa kwa wananchi wa Chake Chake kuwa na sehemu za kujipumzisha na kuogelea. Kwa kulitambua hilo Serikali ndio maana ikajenga upya kiwanja cha Watoto cha Tibirinzi ili kuwawezesha watoto, vijana na wazee kupumzika na kufurahia kwa kupata fursa za michezo mbali mbali. Aidha, mwaka 2015, Serikali kupitia Idara ya Mipango Miji na Vijiji imeandaa Mpango Mkakati wa Uendelezaji Miji ambao pia umehusisha Mji wa Chake Chake. Jambo la msingi linalofuata ni kutayarisha mpango wa kina wa utekelezaji wa Mkakati huo, ambao utazingatia maeneo ya kujipumzisha. Kwa wakati huu Serikali inawaomba wananchi wa Chake Chake kutumia maeneo yaliyokaribu na Mji huo kwa ajili ya kujipumzisha na kuogelea.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Ninashukuru Mhe. Naibu Spika, na ninashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mhe. Naibu Wairi, lakini nilitaka nimwambie Mhe. Naibu Waziri, kwamba kama ulivyokwisha kusema na ndivyo ilivyo Chake Chake ndiyo Mji wa pili katika Zanzibar na maeneo yaliyobakia katika ukanda ambao wa Tibirinzi ndiyo ukanda wa bahari, tukichukulia kwamba hapa Zanzibar tuna Forodhani, wenzetu Tanga wametengeza Forodhani na sisi kule Pemba tunaitaka Forodhani na ukanda uliobakisha ni ule ukanda wa pale Tibirinzi.

Lakini Mhe. Naibu Spika, ninataka nikwambie kwamba, sijui kama ni kweli au si kweli kuwa ule ukanda ambao umepakana na hifadhi ambao ndiyo pale, sijui ninasikia kwamba kweli kumeshatolewa viwanja au laa.

Lakini mimi ninataka nitoe tahadhari ya kwamba kutoka ufukwe mpaka pale hapatimii zaidi ya mita thalathini kama inafika au ishirini. Nikijua kwamba mita kumi na tano ni pekee za barabara kuu, mita zilizobakishwa kumi na tano au kumi ni ambazo ndiyo zenye ufukwe.

Sasa Mhe. Naibu Spika, ninataka nimwambie kwamba ile dhima au dhana nzima iliyokuwepo ya wakati huo ya kufanya pale ni pahala kwa Forodhani au ndiyo watu walipokuwa wanaogolea na sehemu nyengine pameachiwa mikoko namna ile na sasa hivi watu wanataka kupajenga.
Je, Mhe. Naibu Spika, Mhe. Naibu Waziri, unalitolea maamuzi gani; pawe pa viwanja au sehemu ya Forodhani.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Ni kweli sasa hivi katika eneo lile pana shughuli nyingi ambazo zinafanyika, lakini kutokana na mpango mkakati na mpango miji uliopangwa ndani ya Mji wa Chake Chake kuna maeneo mahususi tayari yameshatengwa kwa ajili ya kutengeneza Mji na kwa ajili ya bustani ili watu waweze kupumzika.

Kwa hivyo, naomba avute subra kidogo mpango ule ukamilike ili kwa pamoja tushirikiane katika kuhakikisha kwamba tunaweza kuukuza mji wetu. Lakini kupitia hapa Mhe. Naibu Spika, naomba niwashukuru wananchi wa Jimbo la Chake Chake kupitia kwa Mwakilishi wao Mhe. Suleiman Sarahan Said, kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kuhakikisha kwamba lile suala alilioliuliza kipindi cha kwanza kuhusu mmomonyoko kwenye lile eneo la Ikulu, *ZSFF* pale

ambalo amelizungumza kujitolea kwa wingi kupanda mikoko kwa wingi na sasa hivi eneo lile limekuwa na hifadhi kubwa. (*Makofi*)

Kwa hivyo, naomba washukuru sana wananchi wa Chake Chake kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kuweza kujitolea kwa kushirikiana na Idara yangu ya Mazingira ya kulihifadhi na kulilinda eneo lile. Naomba niwashukuru sana. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri, hakuna swali la nyongeza. Tunaendelea.

Nam. 64

Changamoto za Usalama katika Usafiri wa Anga

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Ndege zinazotoa huduma ya usafiri kwa abiria zimetakiwa kuwa na Rubani (2). Na kwa kuwa Zanzibar inaruhusu kutoa huduma za usafiri wa Anga kwa ndege zenye Rubani mmoja jambo ambalo ni hatari kiusalama na kinyume na Sheria za Anga za Kimataifa.

(a) Je, kwa nini nchi nyengine zimeweza kusimamia Sheria hizo kwa mfano India, Canada, n.k. na kwa nini Zanzibar tunashindwa.

(b) Je, kwa vile kuna kama kesi (3) zimewahi kutokea Rubani akiwa angani na kuugua mfano uwanja wa Mbeya, Iringa na Mwanza, kwa nini Tanzania hatutaki kujifundisha kutokana na matokeo hayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 64 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Sheria ya idadi ya Marubani kuendesha ndege kwa wakati mmoja imeelezwa wazi. Ndege yoyote yenye uzito wa jumla chini ya paundi 12,500 inaweza kuendeshwa na rubani mmoja. Suala la nchi nyingine kuruhusu marubani zaidi ya mmoja, ni la nchi yenyewe na sheria zake. Kama tutaamua kufanya hivyo, litaongeza gharama za uendeshaji kwa mmiliki kutokana na mshahara wa Rubani na upungufu

wa kiti kimoja cha abiria, hivyo, maamuzi haya yataongeza nauli kwa abiria na kuathiri kipato chake.

(b) Utaratibu wa kupima afya kwa marubani ni wa hali ya juu kabisa, hivyo, tukio lolote kuhusu hilo ni nadra sana kutokea na kama linatokea inakuwa ni kudra ya Mwenyezi Mungu. Kinachotakiwa ni kwa vyombo vinavyosimamia taratibu za kiafya kwa Marubani kusimamia kazi zao kwa uadilifu. Ukubwa wa Bima ya mtu ndio inavyomuongoza huduma gani azichukue. Na kwa upande wa haki inapatikana kwa watu wote bila ya kujali uwezo au utashi wa mtu mwenyewe.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri, mimi nilikuwa swali langu niliondoe kama jana lakini mwenzangu hapa Mhe. Nassor Salim Ali, aliuliza jana, jawabu, kipi bora uhai wa binadamu au kulinda gharama za mmiliki wa ndege wakati rubuni ni binadamu na binadamu yeyote lolote linaweza kumtokezea na hana mkataba na Mwenyezi Mungu yule. Hilo la kwanza.

La pili, matukio matatu yaliwahi kutokea rubuni afya yake kuzorota akiwa angani na baadae akatua ndege uwanja wa Mbeya, Mwanza na kwengineko. Yametufundisha nini Mhe. Naibu Waziri, matukio haya.

Jana ulinijibu hapa ukaniambia *DG* wako ana nini na nini, kuwa na digrii, kuwa na diploma si hoja, tunaona Manaibu wengine humu wana digrii, diploma na wanavyojibu tunawaona.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, maswali yake ya nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Kama unavyojua Serikali yoyote ile inajali uhai wa binadamu, hasa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inajua kwamba binaadamu ni muhimu katika kuendeleza maendeleo ya nchi yetu. Sisi tutalichukua suala hili na tutalifikisha panapohusika kwa sababu hili ni jambo la Muungano. Lakini licha ya hivyo, ninamwambia Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwamba, taratibu zimefuatwa katika kutunga sheria hii.

(b) Ameelezea hayo matukio yaliavyotokea na kama nilivyosema mwanzo kwamba, kudra ya Mwenyezi Mungu haiepukiki lakini kila baada ya miezi sita marubani wanakuwa wanapimwa afya zao katika

madaktari ambao waadilifu kabisa na iwapo litatokea hilo basi kama nilivyosema mwanzo ni kudra ya Mwenyezi Mungu.

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru sana na ninamshukuru sana Mhe. Naibu Waziri, kwa majibu mazuri.

Mhe. Naibu Spika, kama utakwenda kwenye rekodi za ajali za ndege zinazotokea duniani, utakuta ndege ambazo zina ma-*pilots* zaidi ya wanne, wawili wanaofanya kazi na wawili kusubiri na bado ajali zinatokea.

Kwa hivyo, suala la kutokea ajali kwenye ndege kuna mambo mengi sana yanatokea. Ni kweli kabisa si vizuri sana ndege ikawa na *pilot* mmoja ninakubali, lakini siyo sababu peke yake ya kwamba ajali hazitotokea. Ndege zote ambazo zimeuwa watu wengi idadi kubwa sana ni ndege ambazo zina marubuni wa kutosha ndani, kuna ma-*engineers* ndani, ni *very high sophisticated equipment*, lakini bado ajali zinatokea.

Lakini ni kweli kabisa kuna umuhimu vile vile wa kuzingatia hayo ambayo Mhe. Naibu Waziri, ameyasema.

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kumuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Naibu Waziri, nauli ya ndege ni shilingi tisini na tano elfu kwenda Pemba kuja Unguja, lakini binadamu huna uwezo wa kumlipa shilingi tisini na tano elfu.

Je, Mhe. Naibu Spika, inapokuwa kama rubuni ni mmoja na hatuombi yatokezee hayo, lakini yakitokezea na kama unavyojua ndege haina konda. Je, huoni ni kuwatia hofu wasafiri wale.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Kama nilivyosema katika majibu yaliyotangulia jibu mama na kama alivyosema Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, kwamba kutokea ajali hili jambo ambalo ni kudra ya Mwenyezi Mungu na kuna ndege ambazo zinakuwa marubuni zaidi ya mmoja na inatokea ajali, lakini nilivyosema mwanzo hizi taratibu na haya mambo yapo katika suala la mambo ya Muungano tumelichukua na kwamba tutalifikisha kwa ajili kulifanyia kazi zaidi.

Nam. 71

Uteuzi wa Wajumbe wa Bodi ya Usajili Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Hivi karibuni iliripotiwa na vyombo mbali mbali vya habari Zanzibar ikiwemo Gazeti la Zanzibar Leo la tarehe 28/7/2016 kuwa Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, amefanya uteuzi wa Wajumbe wa Bodi ya Usajili Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji majengo. Jumla ya Wajumbe walioteuliwa ni sita.

a) Je, uteuzi huo umezingatia vipi masharti ya Sheria ya Wajenzi, Wahandisi na Wakadiriaji majengo No. 5 ya 2008, kuhusu sifa za Wajumbe wa Bodi hiyo.

b) Miongoni mwa Wajumbe walioteuliwa ni wataalamu katika fani za majengo na uhandisi, Je, Mhe. Waziri, amezingatia vipi kumbukumbu za utendaji za wajumbe hao kabla ya kuteuliwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji. kabla sijaanza kujibu maswali ya Mhe. Mwakilishi, lenye kifungu (a) na (b) naomba kutoa maelezo mafupi kuhusu Bodi hii.

Mhe.Spika, Bodi ya Usajili Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo imeundwa rasmi kwa Sheria No. 5 ya mwaka 2008. Majukumu makubwa ya Bodi hii kuratibu na kudhibiti shughuli za Wataalamu (Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo). Aidha, Bodi inawasajili Watalamu hao pamoja na Makampuni ya ushauri *(Consultancy firm)* zinazohusiana na majengo ili

kuhakikisha tunapata wataalamu bora na wanaosimamia majengo kwa viwango bora na hatimae kupata Ujenzi salama.

Mhe. Spika, sasa napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi, masuala yake yenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Bodi ya tatu ya Usajili Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo imeteuliwa rasmi tarehe 28/7/2016 kwa uteuzi wa Wajumbe baada ya uteuzi wa Mwenyekiti uliofanywa na Mhe. Rais, mnamo tarehe 19/05/2016 kwa mujibu wa Sheria ambapo Mkurugenzi anaehusika na shughuli za ujenzi huingia kwenye Bodi kwa mujibu wa wadhifa wake kama inavyoeleza katika kifungu No. 4 cha sheria iliyotajwa hapo juu.

(b) Mhe. Spika, Wajumbe wa Bodi huteuliwa na Waziri baada ya kuangalia na kuridhika sifa na uzoefu wao katika fani ya ujenzi kama ilivyoelezwa katika Sheria No.5, kifungu 4 (c).

Mhe. Spika, Bodi ya Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo ina Mwenyekiti mmoja na Wajumbe sita kama ifuatavyo:-

1. *Arch*.Ashrak M.Hamid - Mwenyekiti
2. *Eng*. Ramadhan M. Bakar - Mjumbe
3. *Arch* Moh'd S.Nassor - Mjumbe
4. *Eng*. Jaffar S. Haji - Mjumbe
5. *Eng*. Ali M. Juma - Mjumbe
6. *Eng*. Laurence A. Gonsalves - Mjumbe
7. Ndg. Ramadhan S. Makame - Mjumbe

Hivyo basi, kumbukumbu za utendaji za wajumbe hao zimeangaliwa vizuri kabla ya kuteuliwa kwao.

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nimuombe tu ndugu yangu, rafiki yangu Mhe. Naibu Waziri, hichi chombo cha Kutunga Sheria na umetaja Sheria hapa Nam. 5 ya kuhusu wakandarasi. Katika wajumbe hao Mhe. Naibu Spika, mmoja hana sifa hiyo.

Katika Wajumbe uliowataja kuna mmoja hana sifa hiyo na hichi chombo ni cha kisheria. Na Sheria inasema kabla ya kuteuwa kwanza awe *consultant quantity*

yule *survivor*, *engineering* au *architect* katika sheria tuliyotaja. Lakini katika mmoja hawa hana uwezo huo na tumeshuhudia ana jengo Serikali imezuia kulipandisha ghorofa na limeshafanya *crack*.

Je, una Bodi nyingi upo tayari kumuhamisha kumpeleka Bodi nyengine. Hii Bodi ina sheria zake kama ulizotaja kwanza *consultant, engineering* au *architect,* lakini katika humu kuna mmoja hana sifa hizo, na ukitaka ushahidi nitakueleza. Ili umtafute pahala kwengine, tunakokwenda ni kwengine dunia nyengine.

Je, upo tayari kumuhamisha kumpeleka kwenye sehemu nyengine kwenye Bodi nyengine. Bodi hii unatakiwa uwe na sifa hizo ulizotaja, kama *consultant*, *architect* au *engineering*. Upo tayari kukaa na Waziri wako kumtafutia pahala pengine kumuweka. Sifa hizi hana mtu huyo na ushahidi utaupata.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Kama nilivyosema kwamba Mhe. Waziri, anapoteuwa Wajumbe huangalia sifa zao na vile vile huangalia ile sekta husika. Huyo Mjumbe aliyemtaja ambayo kutokana ilivyo hatuwezi kumtaja moja kwa moja, lakini ni mjasiria mali katika sekta hii ya ukandarasi. Kwa hivyo, mimi ninamuhakikishia kwamba hizo dhana baadhi ya wakati aziondoshe na kama huo ushahidi upo basi mimi nitamuomba aniletee ofisini ili kuufanyia kazi.

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, Kanuni ya 37, lakini haina haja kusoma, nilichomueleza mimi Mhe. Naibu Waziri, ushahidi ninao nitampa. Nilichomuomba tu siwezi...

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Mhe. Naibu Waziri. amekujibu vizuri sana, amesema kama unao ushahidi ufikishe Ofisini. Nafikiri hakuna zaidi ya hapo.

Nam. 72

Kuanzisha Shirika la Ndege la Zanzibar

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Alijibu:-

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inajitahidi kutafuta vyanzo vipya vya mapato na kuongeza jitihada za ziada za kukusanya mapato na pia kujitangaza zaidi katika ulimwengu huu wa kibiashara.

Je, Serikali imejipangaje kuanzisha Shirika la Ndege la Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said, swali lake Nam. 72 kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, Serikali inatambua kabisa umuhimu wa kuanzisha Shirika la Ndege la Zanzibar kwa lengo la kuimarisha sekta ya usafiri wa anga pamoja na kukuza utalii nchini. Lakini Serikali kwa hivi imejipanga zaidi katika kufanikisha miradi mengine ya kiuchumi na kuendelea kulitumia Shirika la Ndege la Tanzania (*ATC*) katika kujitangaza kwenye ulimwengu wa kibiashara hasa sekta hii ya utalii.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Ninashukuru Mhe. Naibu Spika, na ninamshukuru Mhe. Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri.

Mhe. Naibu Spika, mimi ninachokisema kwamba hii Zanzibar ina visiwa viwili vya Unguja na Pemba na kuna watu siyo kwamba kupanda ndege ni utajiri. Kuna watu matajiri na ndege hawataki kupanda, lakini na kuna watu ambao ni maskini au wako katika hali nyengine wanataka kupanda ndege, lakini kutokana na sekta hii moja kwa moja kuwekwa kwenye sekta binafsi, tiketi zao au bei zao zinapanda kiholela na zinapanda kwa wanavyotaka wenyewe kwa sababu Serikali haina mkono wake katika shirika lile.

Sasa nilikuwa ninamuuliza Mhe. Naibu Waziri, kwamba pamoja na kuwa amesema ana Shirika la Ndege, lakini sijawahi kuona ratiba hata moja inayotoka Dar-es-Salaam kuja Zanzibar, kupitia Pemba kwa Shirika la Ndege la Tanzania.

Lakini ninamuuliza Mhe. Naibu Waziri, pia swali la (b), kwamba yeye ana Wizara yake inayoitwa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji na Kitengo chake kimoja ni Kitengo cha Shirika la Meli. Je, kabla hatujakuwa katika Shirika la Ndege ana Kitengo cha Shirika la Anga angalau tuanzie na hapo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said, maswali yake ya nyongeza yenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Ni kweli kabisa Shirika la Ndege la *ATC* limeanza safari zake Zanzibar na kwa mujibu wa ratiba ilivyopangwa itakuwa inakuja mara tatu mpaka Unguja kupitia Arusha. Lakini kama alivyosema suala la ndege kwenda Pemba hili pia linahitaji kuliangalia zaidi kimkakati wa kibiashara. Lakini suala lake tutalichukua na kulifanyia kazi, lakini kwa hivi sasa Shirika la *Precious Air* nalo linakwenda Pemba, kwa hivyo, linaongeza kuchukua abiria na vile vile kusaidia katika kupunguza nauli za bei za kwenda Pemba.

(b) Nataka kumwambia suala hili tutalichukua na kulifanyia kazi, lakini kwa ufupi ninataka kumwambia kwamba mambo ya anga yote yapo katika mambo ya Muungano.

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, muda wetu wa maswali umekwisha, yaani maswali yetu yamemalizika na leo hatutokuwa na shughuli nyengine zaidi ya hii ambayo tumeimaliza. Kwa hivyo, nitamuomba Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Pili wa Rais, atengue Kanuni ya Muda.

Lakini kabla ya hayo, nilikuwa na matangazo machache naomba niyasome. Matangazo yenyewe ni moja Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari Mhe. Ali Suleiman Ali, anawatangazia Wajumbe wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari kukutana baada ya kumaliza kwa kipindi cha maswali na majibu katika ukumbi wa nambari tatu. Hilo ni suala la kwanza.

Suala la pili, Waheshimiwa, munakumbushwa kuhusiana na semina ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ambayo itakuwepo siku ya Jumapili saa tatu asubuhi tarehe 27/11/2016. Kwa hivyo, nyote munakumbushwa mufike kwa wakati.

Suala la tatu, ni kwamba ratiba ambayo tumepewa mwanzo kabisa itakuwa kidogo ina mabadiliko na Mswada ambao utawekwa mezani Jumatatu utakuwa ni Mswada wa *ZSSF* badala ya Mswada wa Manunuzi halafu baadae ndiyo utakuja kufuata Mswada wa Manunuzi.

Sasa nimuombe Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Pili wa Rais, atutengulie Kanuni ya Muda ili tuweze kumaliza shughuli yetu hii ya leo. Mhe. Waziri karibu.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa shughuli zilizopangwa kufanyika leo zimekamilika na kwa sababu hakuna shughuli nyengine ya Baraza, isipokuwa nikuombe uliahirishe Baraza letu mpaka siku ya Jumatatu asubuhi saa tatu kamili.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

(Saa 5.30 mchana Baraza liliahirishwa hadi
Jumatatu tarehe 28/11/2016 saa 3.00 asubuhi)